SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA MADAKTARI BINGWA WA BINADAMU

Tume ya Utumishi Serikalini kwa niaba ya Wizara ya Afya Zanzibar inatangaza nafasi za kazi za Madaktari bingwa wa Binaadamu.

Utangulizi:

Wizara ya Afya, imeundwa kufuatia mamlaka aliyopewa Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika Sehemu ya tatu, Ibara ya 42(i) ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Kwa mujibu wa kuundwa kwake, Wizara ya Afya, ina majukumu ya kukinga, kutibu na kupambana na maradhi kwa madhumuni ya kuimarisha afya za wananchi wa Zanzibar. Katika kukamilisha majukumu yake Wizara inafuata Sera ya Afya 2011, Mipango Mikatati, Miongozo, Sheria na Kanuni mbali mbali.

Wizara ina lengo kuu la kuimarisha huduma za afya za Kinga na Tiba na kuendelea ustawi wa watu wa Zanzibar na kuhakikisha kwamba, wazanzibari wote wanapata haki ya huduma bora za afya kwa misingi ya usawa kwa kuzingatia viwango na ubora vilivyowekwa kupitia afya ya msingi.

Wizara ya afya inatafuta Madaktari bingwa ambao wana uwezo wa kutoa huduma kwa ufanisi na ili kuweza kuhakikisha Wazanzibari wanapata huduma sahihi kwa wakati.

Nafasi za kazi na Sifa za Wombaji

1. **DAKTARI WA BINADAMU DARAJA LA II KATIKA FANI YA MAGONJWA YA MOYO (CARDIOVASCULAR TECHNOLOGY) Nafasi 2**

Sifa za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya kwanza katika fani ya tiba ya moyo wa binadamu (cardiovascular technology) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa wa moyo na mifumo yake ikiwemo *Echocardiogram, ambulatory electrocardiogram* n.k kulingana na mahitaji ya mgonjwa.
- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya moyo na mengine yasioambukiza.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kutoa tiba ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya Moyo na mifumo yake.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya moyo na mifumo yake ikiwa pamoja na kuipitia upya ili iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

2. **DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MAGONJWA YA MOYO (CARDIOLOGIST) Nafasi 2**

Sifa za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya tiba ya moyo wa binadamu (cardiologist) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) ya kazi katika fani ya *Cardiology*.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa wa moyo na mifumo yake ikiwemo *Echocardiogram, ambulatory electrocardiogram* n.k kulingana na mahitaji ya mgonjwa.
- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya moyo na mengine yasioambukiza.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kutoa tiba ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya Moyo na mifumo yake.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya moyo na mifumo yake ikiwa pamoja na kuipitia upya ili iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

3. **DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MARADHI NA MATATIZO YA MFUMO WA DAMU NA CHEMBE HAI ZAKE (HEMATOLOGIST) Nafasi 1**

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya tiba za maradhi ya mfumo wa damu na chembe hai zake (Hematologist) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) ya kazi katika fani ya *hematology*.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya mfumo wa damu na chembe hai zake na mengine yasioambukiza.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa wa maradhi ya mfumo wa damu na chembe hai zake kama ***bone marrow aspiration na biopsy*** **na** ***peripheral blood smears n.k***
- Kutoa tiba ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa damu na chembe hai za mfumo huo.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya mfumo wa damu na chembe hai za damu ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

4. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA *ORTHOPEDIC*, Nafasi 3

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya tiba za mifupa na ajali (orthopaedic) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) ya kufanya kazi katika fani ya *orthopedic*.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa tiba sahihi za upasuaji wa mifupa ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya viungo (*orthopaedic)* na ajali (trauma) kwa watu wazima na watoto pamoja na kuwashauri wagonjwa juu ya faida na hasara inayoweza kutokea kwa kila aina ya tiba ya upasuaji.
- Kutoa elimu ya afya kwa jamii kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya serikali juu ya madhara yanayotokana na ongezeko la ajali ikiwemo namna bora ya kujikinga na kudhibiti ulemavu na vifo vinavyotokana na ajali.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo yote ya *orthopaedic* ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya, pamoja na kushauri njia sahihi za kuboresha huduma za *orthopedic* Zanzibar.

5. **DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA *INTERNAL MEDICINE (PHYSICIAN).* Nafasi 2**

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Internal Medicine kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili ya kazi katika fani ya *Internal Medicine*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya kuambukiza na yasiyo ambukiza
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi yakuambukiza na yasiyo ambukiza.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

6. **DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA UPASUAJI (GENERAL SURGEON) Nafasi 3**

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya tiba za maradhi ya Upasuaji (General Surgery) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) ya kufanya kazi katika fani ya *General surgery*.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii ikiwemo namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi tofauti ikiwemo saratani.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa.
- Kutoa sahihi za tiba ya upasuaji ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa pamoja na kuwashauri wagonjwa juu ya faida na hasara inayoweza kutokea kwa kila aina ya tiba ya upasuaji.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo yote ya *upasuaji* ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya, pamoja na kushauri njia sahihi za kuboresha huduma za *orthopedic* Zanzibar.

7. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MAGONJWA YA KINA MAMA (OBSTETRIC AND GYNACOLOGIST)

Nafasi 3.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Obstetric and Gynacology kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Obstetric and Gynacology*.

- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi tofauti ya akina mama na sababu na namna ya kuepuka matatizo yanayojitokeza wakati wa uja uzito ambayo husababisha magonjwa na vifo kwa mama na mtoto.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa matatizo ya wanawake, mama wajawazito na watoto wachanga.
- Kutoa tiba ikiwemo za kibingwa pamoja na za upasuaji kwa matatizo ya wanawake na mama wajawazito.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya wanawake, mama wajawazito na watoto wachanga ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

8. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MAGONJWA YA MAFIGO (NEPHROLOGIST) Nafasi 2.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Magonjwa ya mafigo (Nephrology) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili wa kufanya kazi katika fani ya *Nephrology.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi tofauti ya mafigo.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa matatizo ya mafigo.
- Kutoa tiba za kibingwa ikiwemo za usafishaji mafigo (dialysis) na upasuaji kwa matatizo ya mafigo.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya mafigo ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya.

9. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MAGONJWA YA MACHO (OPHTHALMOLOGIST) Nafasi 2.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Magonjwa ya macho (Ophthalmoloist) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili wa kufanya kazi katika fani ya *ophthalmology.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi tofauti ya macho.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa matatizo ya macho.

- Kutoa tiba za kibingwa ikiwemo na za upasuaji kwa matatizo ya macho.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya macho ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya na kushauri namna bora ya kuimarisha huduma za matibabu ya macho Zanzibar.

10. DAKTARI WA BINADAMU KATIKA FANI YA MAGONJWA YA MACHO (OPTOMETRIST) Nafasi 1.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya kwanza katika fani ya Magonjwa ya macho (Optometry) kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua mwaka mmoja wa kufanya kazi katika fani ya *optometry.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi tofauti ya macho.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa matatizo ya macho.
- Kufanya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa wa macho ikiwemo Kupima watu wenye uoni hafifu na kuwapa miwani stahiki.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.

- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi na matatizo ya macho ikiwa pamoja na kuipitia upya iendane na wakati.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya na kushauri namna bora ya kuimarisha huduma za matibabu ya macho Zanzibar.

11. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MAGONJWA YA TIBA ZA DHARURA (EMERGENCY PHYSICIAN) Nafasi 4.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Emergency Medicine kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwil (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Emergency Medicine*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya kuambukiza na yasiyo ambukiza.
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program) ikiwemo namna ya kugundua dalili za magonjwa wa dharura, hatua za kuchukua katika kupata huduma ya kwanza na kuwahi hospitali mapema.
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo vya haraka na vya kawaida kwa wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi ikiwemo za kibingwa za dharura na za kawaida kwa wagonjwa.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.

- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya magonjwa ya dharura ya kuambukiza na yasiyo ambukiza.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya na kushauri namna bora ya kuimarisha huduma za tiba za dharura Zanzibar.

12. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA MARADHI YA NGOZI *(DERMATOLOGIST)* Nafasi 2.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Dermatology kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Dermatology*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na kudhibiti maradhi ya ngozi ya kuambukiza na yasiyo ambukiza
- Kutoa huduma za afya kwenye jamii (outreach program)
- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa wenye maradhi tofauti ya ngozi.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo ya Kinga na tiba sahihi ya maradhi tofauti ya ngozi.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya ya maradhi ya ngozi.

13. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA I KATIKA FANI YA UCHUNGUZI KWA NJIA YA MIONZI *(RADIOLOGIST)* Nafasi 2.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Radiolojia kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua mwaka mmoja wa kufanya kazi katika fani ya *Radiology.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi ikiwemo wa kibingwa na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa pamoja na kushauriana na madaktari wengine juu ya uchunguzi sahihi wa mgonjwa.
- Kutoa tiba sahihi ikiwemo za kibingwa kwa wagonjwa ikiwemo wakati wa uchunguzi.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wafanyakazi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo sahihi ya uchunguzi wa maradhi tofauti.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya katika uchunguzi wa maradhi.

14. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA KWANZA KATIKA FANI YA MARADHI YA MFUMO WA MKOJO *(UROLOGIST)* Nafasi 3

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Urology kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya Urology.
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi ikiwemo wa kibingwa na kutafsiri vipimo kwa wagonjwa pamoja na kushauriana na madaktari wengine juu ya uchunguzi sahihi wa mgonjwa.
- Kutoa tiba sahihi za kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa mkojo kwa watoto na watu wazima ikiwemo huduma za upasuaji.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo sahihi ya uchunguzi wa maradhi tofauti.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya katika uchunguzi wa maradhi.

15. **DAKTARI WA BINADAMU DARAJA LA II KATIKA FANI YA USINGIZI *(ANAESTHESIOLOGIST)* Nafasi 2.**

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Anaesthesia kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Anesthesia.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi ikiwemo wa kibingwa kwa wagonjwa wa usingizi pamoja na wagonjwa mahututi *(intensive care services)* ikiwemo kushauriana na madaktari wengine juu ya njia sahihi za upasuaji wa wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi za kibingwa kwa wagonjwa.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo sahihi ya uchunguzi wa maradhi tofauti.

- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya katika uchunguzi wa maradhi.

16. **DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA KWANZA KATIKA FANI YA USINGIZI *(ANAESTHESIOLOGIST)* Nafasi 4.**

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya Anaesthesia kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Anesthesia.*
- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi ikiwemo wa kibingwa kwa wagonjwa wa usingizi pamoja na wagonjwa mahututi *(intensive care services)* ikiwemo kushauriana na madaktari wengine juu ya njia sahihi za upasuaji wa wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi za kibingwa kwa wagonjwa.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo sahihi ya uchunguzi wa maradhi tofauti.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya katika uchunguzi wa maradhi.

17. DAKTARI BINGWA WA BINADAMU DARAJA LA KWANZA KATIKA FANI YA MISHIPA YA FAHAMU *(NEUROLOGIST)* Nafasi 2.

Sifa Za Muombaji:

- Awe mwenye shahada ya pili (uzamili) katika fani ya **Neurology** kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya *Anesthesia.*

- Awe na Leseni hai.

Majukumu:

- Kuwaona na kuwasikiliza wagonjwa, Kufanya uchunguzi ikiwemo wa kibingwa kwa wagonjwa wenye matatizo ya mishipa ya fahamu (Neurology) ikiwemo kushauriana na madaktari wengine juu ya njia sahihi za matibabu ya wagonjwa.
- Kutoa tiba sahihi za kibingwa ikiwemo kutasfiri vipimo.
- Kusimamia na kufundisha wafanyakazi na wanafunzi walio chini yake pamoja na kufanya tafiti.
- Kuandaa Miongozo sahihi ya uchunguzi wa maradhi tofauti.
- Kupanga, kufanya tathmini na kuandaa mpango wa makisio ya bajeti ya huduma za afya katika uchunguzi wa maradhi.

Jinsi ya kuomba:

- Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

KATIBU,

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,

S.L.P 1587,

ZANZIBAR.

- Hati zote zitakazounganishwa na maombi ya ajira zitumwe katika muundo wa **PDF** kwenye email ifuatayo maombismz@zanajira.go.tz kuanzia tarehe 27 Januari, 2023 hadi tarehe 18 Febuari, 2023.